# Mika

1 Neno la Mwenyezi Mungu lilimjia Mika
Mmoreshethi wakati wa utawala wa Yothamu,
Ahazi na Hezekia, wafalme wa Yuda, ufunuo
aliouona kuhusu Samaria na Yerusalemu.

2 Sikieni, enyi mataifa, enyi nyote,
sikilizeni, ee dunia na wote mliomo,
ili Bwana Mungu Mwenyezi ashuhudie dhidi yenu,
Bwana kutoka Hekalu lake takatifu.

*Hukumu dhidi ya Samaria na Yerusalemu*

3 Tazama! Mwenyezi Mungu anakuja kutoka mahali pake;
anashuka na kukanyaga
mahali palipoinuka juu pa dunia.
4 Milima inayeyuka chini yake
na mabonde yanagawanyika
kama nta mbele ya moto,
kama maji yanayotiririka kasi
kwenye mteremko.
5 Yote haya ni kwa sababu ya kosa la Yakobo,
ni kwa sababu ya dhambi za nyumba ya Israeli.
Kosa la Yakobo ni lipi?
Je, sio Samaria?
Je, mahali pa juu pa Yuda pa kuabudia ni nini?
Je, sio Yerusalemu?

6 “Kwa hiyo nitaufanya Samaria kuwa lundo la kokoto,
mahali pa kuotesha mizabibu.
Nitayamwaga mawe yake katika bonde
na kuacha wazi misingi yake.
7 Sanamu zake zote
zitavunjwa vipande vipande;
zawadi zake zote za Hekalu
zitachomwa kwa moto;
nitaharibu vinyago vyake vyote.
Kwa kuwa alikusanya zawadi zake
kutokana na ujira wa kahaba,
nazo zitatumika tena
kulipa mishahara ya kahaba.”

### *Kulia na kuomboleza*

8 Kwa ajili ya hili nitalia na kuomboleza;
nitatembea bila viatu na tena uchi.
Nitabweka kama mbweha
na kuomboleza kama bundi.
9 Kwa sababu jeraha lake halitibiki;
limekuja kwa Yuda.
Limefika hasa kwenye lango la watu wangu,
hata Yerusalemu kwenyewe.
10 Usiliseme hili huko Gathi;
usilie hata kidogo.
Huko Beth-le-Afra
gaagaa mavumbini.
11 Piteni mkiwa uchi na wenye aibu,
ninyi mnaoishi Shafiri.
Wale wanaoishi Saanani
hawatatoka nje.
Beth-Eseli iko katika maombolezo;
kinga yake imeondolewa kwako.

12 Wale wanaoishi Marothi wanagaagaa kwa maumivu
wakingoja msaada,
kwa sababu maangamizi yamekuja
kutoka kwa Mwenyezi Mungu,
hata katika lango la Yerusalemu.
13 Enyi mnaoishi Lakishi,
fungeni farasi kwenye magari ya vita.
Mlikuwa chanzo cha dhambi
kwa Binti Sayuni,
kwa kuwa makosa ya Israeli
yalikutwa kwako.
14 Kwa hiyo utaipa Moresheth-Gathi
zawadi za kuagana.
Mji wa Akzibu utaonesha wazi udanganyifu
kwa wafalme wa Israeli.
15 Nitawaleteeni atakayewashinda
ninyi mnaoishi Maresha.
Yeye aliye utukufu wa Israeli
atakuja Adulamu.
16 Nyoeni nywele zenu katika kuomboleza
kwa ajili ya watoto wenu mnaowafurahia;
jifanyieni upara kama tai,
kwa kuwa watawaacha
na kwenda uhamishoni.

# 2

*Mipango ya mwanadamu na mipango ya Mwenyezi Mungu*

1 Ole kwa wale wapangao uovu,
kwa wale wapangao hila vitandani mwao!
Kunapopambazuka wanalitimiza

kwa sababu uko katika uwezo wao
kutekeleza.
2 Wanatamani mashamba na kuyakamata,
pia nyumba na kuzichukua.
Wanamlaghai mwanaume nyumba yake,
mwanadamu mwenzake urithi wake.
3 Kwa hiyo, Mwenyezi Mungu asema:
"Ninapanga maangamizi dhidi ya watu hawa,
ambayo hamwezi kujiokoa wenyewe.
Hamtatembea tena kwa majivuno,
kwa kuwa utakuwa ni wakati wa maafa.
4 Siku hiyo watu watawadhihaki,
watawafanyia mzaha
kwa wimbo huu wa maombolezo:
'Tumeangamizwa kabisa;
mali ya watu wangu imegawanywa.
Ameninyang'anya!
Ametoa mashamba yetu kwa wasaliti.' "

5 Kwa hiyo hutakuwa na yeyote katika kusanyiko
la Mwenyezi Mungu
wa kugawanya mashamba kwa kura.

### *Manabii wa uongo*

6 Manabii wao husema, "Usitabiri.
Usitabiri kuhusu vitu hivi;
aibu haitatupata."
7 Je, ingesemwa, ee nyumba ya Yakobo:
"Je, Roho wa Mwenyezi Mungu amekasirika?
Je, yeye hufanya vitu kama hivyo?"

"Je, maneno yangu hayamfanyii mema
yeye ambaye njia zake ni nyofu?
8 Siku hizi watu wangu wameinuka

kama adui.
Unawavua joho la kitajiri wale wanaopita
pasipo kujali,
kama watu warudio kutoka vitani.
9 Unawahamisha wanawake wa watu wangu
kutoka nyumba zao za kupendeza.
Unaondoa baraka yangu
kwa watoto wao milele.
10 Inuka, nenda zako!
Kwa maana hapa sio mahali pako pa kupumzikia,
kwa sababu pametiwa unajisi,
pameharibiwa, wala hapatengenezeki tena.
11 Ikiwa mwongo na mdanganyifu atakuja na kusema,
'Nitawatabiria divai na pombe kwa wingi,'
angekuwa ndiye nabii
anayekubalika na watu hawa!

### *Ahadi ya ukombozi*

12 "Hakika nitawakusanya ninyi nyote, ee Yakobo,
Hakika nitawaleta pamoja mabaki ya Israeli.
Nitawaleta pamoja kama kondoo ndani ya zizi,
kama kundi kwenye malisho yake,
mahali hapa patakuwa na msongamano wa watu.
13 Yeye afunguaye njia atawatangulia;
watapita kwenye lango na kutoka nje.
Mfalme wao atawatangulia,
Mwenyezi Mungu atakuwa kiongozi."

# 3

### *Viongozi na manabii wakemewa*

1 Kisha nikasema,

“Sikilizeni enyi viongozi wa Yakobo,
enyi watawala wa nyumba ya Israeli.
Je, hampaswi kujua hukumu,
2 ninyi mnaochukia mema
na kupenda maovu;
ninyi mnaowachuna watu wangu ngozi
na kuondoa nyama kwenye mifupa yao;
3 ninyi mnaokula nyama ya watu wangu,
mnaowachuna ngozi
na kuvunja mifupa yao vipande vipande;
mnaowakatakata kama nyama
ya kuwekwa kwenye sufuria
na kama nyama
ya kuwekwa kwenye chungu?”

4 Kisha watamlilia Mwenyezi Mungu,
lakini hatawajibu.
Wakati huo atawaficha uso wake
kwa sababu ya uovu waliotenda.
5 Hili ndilo asemalo Mwenyezi Mungu:
“Kuhusu manabii wanaowapotosha watu wangu,
mtu akiwalisha,
wanatangaza ‘amani’;
kama hakufanya hivyo,
wanaandaa kupigana vita dhidi yake.
6 Kwa hiyo usiku utawajieni, msiweze kuwa na maono,
na giza, msiweze kubashiri.
Jua litawachwea manabii hao,
nao mchana utakuwa giza kwao.
7 Waonaji wataaibika
na waaguzi watafedheheka.
Wote watafunika nyuso zao

kwa sababu hakuna jibu litokalo kwa Mungu."
8 Lakini mimi nimejazwa nguvu,
nimejazwa Roho wa Mwenyezi Mungu,
haki na uweza,
kumtangazia Yakobo kosa lake,
na Israeli dhambi yake.

9 Sikieni hili, enyi viongozi wa nyumba ya Yakobo,
enyi watawala wa nyumba ya Israeli,
mnaodharau haki
na kupotosha kila lililo sawa;
10 mnaojenga Sayuni kwa kumwaga damu
na Yerusalemu kwa uovu.
11 Viongozi wake wanahukumu kwa rushwa,
na makuhani wake wanafundisha kwa malipo,
nao manabii wake wanatabiri kwa fedha.
Hata hivyo wanamwegemea Mwenyezi Mungu na kusema,
"Je, Mwenyezi Mungu si yumo miongoni mwetu?
Hakuna maafa yatakayotupata."
12 Kwa ajili yenu,
Sayuni italimwa kama shamba,
Yerusalemu itakuwa lundo la kokoto,
na kilima cha Hekalu
kitakuwa kichuguu
kilichofunikwa na vichaka.

# 4

*Mlima wa Mwenyezi Mungu*
*(Isaya 2:2-4)*

1 Katika siku za mwisho
mlima wa Hekalu la Mwenyezi Mungu utaimarishwa
kama mlima mkuu miongoni mwa milima yote;
utainuliwa juu ya vilima,
na watu wa mataifa watamiminika humo.
2 Mataifa mengi yatakuja na kusema,
“Njooni, twendeni kwenye mlima wa Mwenyezi Mungu,
kwenye nyumba ya Mungu wa Yakobo.
Atatufundisha njia zake,
ili tuweze kuenenda katika mapito yake.”
Torati itatoka Sayuni,
neno la Mwenyezi Mungu litatoka Yerusalemu.
3 Atahukumu kati ya mataifa mengi,
na ataamua migogoro ya mataifa
yenye nguvu na yaliyo mbali.
Watafua panga zao ziwe majembe,
na mikuki yao kuwa miundu ya kukata matawi.
Taifa halitainua upanga dhidi ya taifa jingine,
wala hawatajifunza vita tena.
4 Kila mtu ataketi chini ya mzabibu wake
na chini ya mtini wake,
wala hakuna mtu atakayewaogopesha,
kwa kuwa Mwenyezi Mungu,
Mungu wa majeshi ya mbinguni amesema.
5 Mataifa yote yanaweza kutembea
katika jina la miungu yao;
sisi tutatembea katika jina la Mwenyezi Mungu,
Mungu wetu milele na milele.

### *Mpango wa Mwenyezi Mungu*

6 “Katika siku hiyo,” asema Mwenyezi Mungu,
“nitawakusanya walemavu;
nitawakusanya walio uhamishoni
na wale niliowahuzunisha.
7 Nitawafanya walemavu kuwa mabaki,
wale waliofukuzwa kuwa taifa lenye nguvu.
Mwenyezi Mungu atawatawala katika Mlima Sayuni
kuanzia siku hiyo na hata milele.
8 Lakini kwako wewe, ee mnara wa ulinzi wa kundi,
ee ngome ya Binti Sayuni,
milki ya awali itarudishwa kwako,
ufalme utakuja kwa Binti Yerusalemu.”

9 Kwa nini sasa unalia kwa nguvu:
kwani huna mfalme?
Je, mshauri wako amekufa, hata maumivu yakukamate
kama ya mwanamke
aliye na uchungu wa kuzaa?
10 Gaagaa kwa uchungu, ee Binti Sayuni,
kama mwanamke mwenye uchungu wa kuzaa,
kwa kuwa sasa ni lazima uuache mji
ukapige kambi uwanjani.
Utaenda Babeli;
huko utaokolewa.
Huko Mwenyezi Mungu atakukomboa
kutoka mikononi mwa adui zako.

11 Lakini sasa mataifa mengi
yamekusanyika dhidi yako.

Wanasema, “Mwache anajisiwe,
macho yetu na yatazame Sayuni kwa furaha!”
12 Lakini hawayajui
mawazo ya Mwenyezi Mungu;
hawauelewi mpango wake,
yeye awakusanyaye kama miganda
kwenye sakafu ya kupuria.
13 “Inuka upure, ee Binti Sayuni,
kwa kuwa nitakupa pembe za chuma;
nitakupa kwato za shaba
na utavunja vipande vipande mataifa mengi.”
Utatoa mapato yao waliopata kwa udanganyifu kwa Mwenyezi Mungu,
utajiri wao kwa Bwana wa dunia yote.

# 5

## *Mtawala aliyeahidiwa kutoka Bethlehemu*

1 Panga majeshi yako, ee mji wa majeshi,
kwa kuwa kuzingirwa kumepangwa dhidi yetu.
Watampiga mtawala wa Israeli
shavuni kwa fimbo.

2 “Lakini wewe, Bethlehemu Efrata,
ingawa u mdogo miongoni mwa koo za Yuda,
kutoka kwako atatokea kwa ajili yangu
yeye atakayekuwa mtawala katika Israeli,
ambaye asili yake ni kutoka zamani,
kutoka milele.”

3 Kwa hiyo Israeli utaachwa

hadi mwanamke aliye na uchungu
atakapozaa mwana,
na ndugu zake wengine warudi
kujiunga na Waisraeli.

4 Atasimama na kulichunga kundi lake
katika nguvu ya Mwenyezi Mungu,
katika utukufu wa jina la Mwenyezi Mungu,
Mungu wake.
Nao wataishi kwa usalama, kwa kuwa wakati
huo
ukuu wake utaenea hadi miisho ya dunia.
5 Naye atakuwa amani yao.

*Ukombozi na uharibifu*

Mwashuru atakapovamia nchi yetu
na kupita katika ngome zetu,
tutawainua wachungaji saba dhidi yake,
hata viongozi wanane wa watu.
6 Wataitawala nchi ya Ashuru kwa upanga,
nchi ya Nimrodi kwa upanga.
Atatuokoa kutoka kwa Mwashuru
atakapoivamia nchi yetu
na kuingia katika mipaka yetu.

7 Mabaki ya Yakobo yatakuwa
katikati ya mataifa mengi
kama umande kutoka kwa Mwenyezi Mungu,
kama manyunyu juu ya majani,
ambayo hayamngoji mtu
wala kukawia kwa mwanadamu.
8 Mabaki ya Yakobo yatakuwa miongoni mwa
mataifa,
katikati ya mataifa mengi,

kama simba miongoni mwa wanyama wa msituni,
kama mwana simba miongoni
mwa makundi ya kondoo,
ambaye anaumiza vibaya na kuwararua
kila anapopita katikati yao,
wala hakuna awezaye kuokoa.
9 Mkono wako utainuliwa juu kwa ushindi juu ya watesi wako,
nao adui zako wote wataangamizwa.
10 “Katika siku ile,” asema Mwenyezi Mungu,
“nitaangamiza farasi wenu kati yenu,
na kubomoa magari yenu ya vita.
11 Nitaiangamiza miji ya nchi yenu,
na kuziangusha chini ngome zenu zote.
12 Nitaangamiza uchawi wenu,
na hamtapiga tena ramli.
13 Nitaangamiza sanamu zenu,
na mawe yenu ya ibada yatoke kati yenu;
hamtasujudia tena
kazi ya mikono yenu.
14 Nitang’oa nguzo za Ashera kati yenu,
na kubomoa miji yenu.
15 Nitalipiza kisasi kwa hasira na ghadhabu,
kwa mataifa ambayo hayajanitii.”

# 6

### *Shtaka la Mwenyezi Mungu dhidi ya Israeli*

1 Sikiliza asemalo Mwenyezi Mungu:
“Simama, jitetee mbele ya milima;
vilima na visikie lile unalotaka kusema.

2 “Sikilizeni, ee milima, mashtaka ya Mwenyezi Mungu,
sikilizeni, enyi misingi ya milele ya dunia.
Kwa kuwa Mwenyezi Mungu ana shauri dhidi ya watu wake;
anatoa mashtaka dhidi ya Israeli.

3 “Watu wangu, nimewatendea nini?
Nimewalemea kwa jinsi gani? Mnijibu.
4 Nimewatoa kutoka Misri na kuwakomboa
kutoka nchi ya utumwa.
Nilimtuma Musa awaongoze,
pia Haruni na Miriamu.
5 Watu wangu, kumbukeni jinsi Balaki mfalme wa Moabu
alivyofanya shauri
na kile Balaamu mwana wa Beori alichojibu.
Kumbukeni safari yenu kutoka Shitimu hadi Gilgali,
ili mfahamu matendo ya haki ya Mwenyezi Mungu.”

6 Nimjie Mwenyezi Mungu na kitu gani na kusujudu
mbele za Mungu aliyetukuka?
Je, nije mbele zake na sadaka za kuteketezwa,
nije na ndama za mwaka mmoja?
7 Je, Mwenyezi Mungu atafurahishwa na kondoo dume elfu,
au mito elfu kumi ya mafuta?
Je, nimtoe mzaliwa wangu wa kwanza
kwa ajili ya kosa langu,
mtoto wangu mwenyewe

kwa ajili ya dhambi ya nafsi yangu?
8 Amekuonesha yaliyo mema, ee mwanadamu.
Mwenyezi Mungu anataka nini kwako?
Ila kutenda kwa haki na kupenda rehema,
na kwenda kwa unyenyekevu na Mungu wako.

### *Hatia na adhabu ya Israeli*

9 Sikiliza! Mwenyezi Mungu anauita mji:
kulicha jina lako ni hekima:
“Tii hiyo fimbo na yeye aliyeiamuru.
10 Je, bado nisahau, ee nyumba ya uovu,
hazina yako uliyopata kwa udanganyifu
na vipimo vilivyopunguka,
ambavyo vimelaaniwa?
11 Je, naweza kuhukumu kuwa
mtu mwenye mizani ya udanganyifu hana hatia,
aliye na mfuko wa mawe ya kupimia ya uongo?
12 Matajiri wake ni wajeuri;
watu wake ni waongo
na ndimi zao zinazungumza
kwa udanganyifu.
13 Kwa hiyo, nimeanza kukuharibu,
kuwaangamiza kwa sababu ya dhambi zenu.
14 Mtakula lakini hamtashiba;
tumbo zenu bado zitakuwa tupu.
Mtaweka akiba lakini hamtaokoa chochote,
kwa sababu mtakachoweka akiba
nitatoa kwa upanga.
15 Mtapanda lakini hamtavuna;
mtakamua zeituni lakini
hamtatumia mafuta yake.

Mtakamua zabibu
lakini hamtakunywa hiyo divai.
16 Mmezishika sheria za Omri
na matendo yote ya nyumba ya Ahabu,
tena umefuata desturi zao.
Kwa hiyo nitakutoa kwa maangamizi
na watu wako kuwa dhihaka;
mtachukua dharau za mataifa."

# 7

*Taabu ya Israeli*

1 Taabu gani hii niliyo nayo!
Nimefanana na yule akusanyaye
matunda ya kiangazi,
aokotaye masazo baada ya kuvunwa
shamba la mizabibu;
hakuna kishada chenye matunda ya kula,
hakuna hata ile tini ya mwanzoni ninayoitamani.
2 Wanaomcha Mungu wameondolewa kutoka nchi;
hakuna mtu mnyofu hata mmoja aliyebaki.
Watu wote wanavizia kumwaga damu,
kila mmoja anamwinda ndugu yake kwa wavu.
3 Mikono yote miwili ni hodari katika kufanya ubaya,
mtawala anadai zawadi,
hakimu anapokea rushwa,
wenye nguvu wanaamuru wanachotaka:
wote wanapanga njama pamoja.
4 Aliye mwema kupita wote kati yao
ni kama mchongoma,
anayeonekana mnyofu zaidi miongoni mwao

ni mbaya kuliko uzio wa miiba.
Siku ya walinzi wako imewadia,
siku Mungu atakayokutembelea.
Sasa ni wakati wao
wa kuchanganyikiwa.
5 Usimtumaini jirani;
usiweke matumaini kwa rafiki.
Hata kwa yule alalaye kifuani mwako
uwe mwangalifu kwa maneno yako.
6 Kwa kuwa mwana humdharau baba yake,
naye binti huinuka dhidi ya mama yake,
mkwe kuwa kinyume na mama mkwe wake:
adui wa mtu ni wale wa nyumbani mwake hasa.

7 Lakini mimi, namtazama Mwenyezi Mungu kwa matumaini,
namngoja Mungu Mwokozi wangu;
Mungu wangu atanisikia mimi.

### *Israeli atainuka*

8 Usifurahie msiba wangu, ee adui yangu!
Ingawa nimeanguka, nitainuka.
Japo ninaketi gizani,
Mwenyezi Mungu atakuwa nuru yangu.
9 Kwa sababu nimetenda dhambi dhidi yake,
nitabeba ghadhabu ya Mwenyezi Mungu,
hadi atakapotetea shauri langu
na kuithibitisha haki yangu.
Atanileta nje kwenye mwanga,
nami nitaiona haki yake.
10 Kisha adui yangu ataliona
naye atafunikwa na aibu,
yule aliyeniambia,

"Yu wapi Mwenyezi Mungu, Mungu wako?"
Macho yangu yataona kuanguka kwake,
hata sasa atakanyagwa chini ya mguu
kama tope barabarani.

11 Siku ya kujenga kuta zako itawadia,
siku ya kupanua mipaka yako.
12 Siku hiyo watu watakuja kwako
kutoka Ashuru na miji ya Misri,
hata kutoka Misri hadi Mto Frati,
na kutoka bahari hadi bahari,
na kutoka mlima hadi mlima.
13 Dunia itakuwa ukiwa kwa sababu ya wakazi wake,
kwa sababu ya matunda ya matendo yao.

*Sala na sifa*

14 Wachunge watu wako kwa fimbo yako,
kundi la urithi wako,
ambalo linaishi peke yake msituni,
katika maeneo ya malisho yenye rutuba.
Waache walishe katika Bashani na Gileadi
kama ilivyokuwa siku za kale.

15 "Kama siku zile mlipotoka Misri,
nitawaonesha maajabu yangu."

16 Mataifa yataona na kuaibika,
waliondolewa nguvu zao zote.
Wataweka mikono yao kwenye vinywa vyao
na masikio yao yatakuwa na uziwi.
17 Wataramba mavumbi kama nyoka,
kama viumbe vinavyotambaa ardhini.
Watatoka nje ya mapango yao wakitetemeka;

watamgeukia Mwenyezi Mungu, Mungu wetu, kwa hofu
nao watakuogopa.
18 Ni nani Mungu kama wewe,
ambaye anaachilia dhambi
na kusamehe makosa
ya mabaki ya urithi wake?
Wewe huwi na hasira milele,
bali unafurahia kuonesha rehema.
19 Utatuhurumia tena,
utazikanyaga dhambi zetu
chini ya nyayo zako,
na kutupa maovu yetu yote
katika vilindi vya bahari.
20 Utakuwa wa kweli kwa Yakobo,
nawe utamwonesha Ibrahimu rehema,
kama ulivyowaahidi kwa kiapo baba zetu
siku za kale.

# Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu

## The Holy Bible in Swahili: Open Neno: Maandiko Matakatifu 2024

copyright © 2018, 2024 Biblica, Inc.

Language: Kiswahili (Swahili)

Contributor: Biblica, Inc.

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™
Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.
Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™
Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

**Creative Commons License**

Kazi hii imewezeshwa kupitia idhini ya kundi la the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). Ili kuona nakala ya idhini hii, angalia kwenye anwani tovuti ya http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 au uandike barua kwa Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® ni alama ya biashara iliyosajilishwa na shirika la Biblica, Inc; unahitaji ruhusa ya kimaandiko kutoka kwa Biblica, Inc. ili kutumia alama ya biashara ya Biblica®. Kulingana na makubaliano ya leseni ya CC BY-SA, unaweza kutoa nakala na kusambaza kazi hii bila kuibadilisha kamwe, mradi tu udumishe alama ya biashara ya Biblica®. Ukibadilisha au kufasiri kazi hii, na hivyo ukanyambua kazi tofauti, sharti uondoe alama ya biashara ya Biblica®. Katika kazi uliyonyambua, sharti uarifu mabadiliko yako, na kutambua kazi yako hivi: "Kazi ya asili ya Biblica, Inc. inapatikana bila bei katika tovuti zawww.biblica.com na open.bible." Ilani ya hakimiliki sharti iwe katika ukurasa wa kichwa au wa hakilimiliki kama ifuatavyo:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™
Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.
Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™
Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

"Biblica" ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

"Biblica" is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

Sharti pia uwasilishe kazi uliyonyambua kupitia kwa liseni hiyo hiyo ya CC BY-SA.

Ikiwa ungependa kujulisha Biblica, Inc. kuhusu tafsiri yako ya kazi hii, tafadhali wasiliana nasi katika tovuti https://open.bible/contact-us.

This work is made available under the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). To view a copy of this license, visit http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 or send a letter to Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® is a trademark registered by Biblica, Inc., and use of the Biblica® trademark requires the written permission of Biblica, Inc. Under the terms of the CC BY-SA license, you may copy and redistribute this unmodified work as long as you keep the Biblica® trademark intact. If you modify a copy or translate this work, thereby creating a derivative work, you must remove the Biblica® trademark. On the derivative work, you must indicate what changes you have made and attribute the work as follows: "The original work by Biblica, Inc. is available for free atwww.biblica.com and open.bible."

Notice of copyright must appear on the title or copyright page of the work as follows:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™

Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.

Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™

Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

"Biblica" ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

"Biblica" is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

You must also make your derivative work available under the same license (CC BY-SA).

If you would like to notify Biblica, Inc. regarding your translation of this work, please contact us at https://open.bible/contact-us.

This translation is made available to you under the terms of the Creative Commons Attribution Share-Alike license 4.0.

You have permission to share and redistribute this Bible translation in any format and to make reasonable revisions and adaptations of this translation, provided that:

You include the above copyright and source information.

- If you make any changes to the text, you must indicate that you did so in a way that makes it clear that the original licensor is not necessarily endorsing your changes.
- If you redistribute this text, you must distribute your contributions under the same license as the original.

Pictures included with Scriptures and other documents on this site are licensed just for use with those Scriptures and documents. For other uses, please contact the respective copyright owners.

Note that in addition to the rules above, revising and adapting God's Word involves a great responsibility to be true to God's Word. See Revelation 22:18-19.

2025-05-21

---

PDF generated using Haiola and XeLaTeX on 20 May 2025 from source files dated 21 May 2025

72687ba8-7233-577d-bf23-786df16f869d